



HAYATI SALIM ALI KIBAO

Hayati Salim Ali Kibao alizaliwa mwaka 1933 katika kijiji cha Mnyanjani, nje kidogo ya mji wa Tanga. Mwaka 1943 alianza shule ya msingi na alipofika darasa la tatu mwaka 1945 mjimi Mwanza aliachishwa shule na marehemu baba yake Sh. Ali bin Hemed (Kibao) ili amsaidie kazi za nyumbani pamoja na kumfundisha ilimu na dini ya Kiislamu. Mwaka 1947, mwezi Mei, alifundishwa kazi ya ushoni wa nguo kwa fundi Amuri Jirini baada ya kurejea Tanga. Baada ya kufuzu ufundi wa kushona nguo alikwenda tena Mwanza mwaka 1949 hadi 1953.

Mwaka 1954 alihamia Kamachumu, Bukoba. Kutoka Kamachumu alikwenda kuishi Mombasa Kenya hadi mwaka 1970 huku akiwa na kazi yake ya ushoni. Hayati Kibao alikuwa mtunzi na mwandishi wa fasihi ya Kiswahili, mtetezi wa Kiswahili, mshiriki wa vipindi vya Kiswahili radioni, mwandishi wa makala ya Kiswahili kuhusu matumizi na maana za maneno ya Kiswahili alianza harakati za Kiswahili kwa kutunga mashairi na tenzi kati ya mwaka 1955 na 1956. Changamoto ya utunzi aliipata kwa marehemu babu yake mzaa baba, Mzee Hemed Abdallah, aliyekuwa mahiri wa tenzi, mashairi na hadithi. Babu yake huyo alifariki mwaka 1928, na Kibao alipata changamoto kutoka katika vitabu vya tenzi vya hayati babu yake.

Baadhi ya vitabu vya babu yake ni tenzi za *Abdulrahman na Sufiani*, *Vita vya Wadachi Kutamalaki Mrima* na vinginevyo ambavyo havikupata kuchapishwa. Kitabu cha kwanza cha Marehemu Salimu Ali Kibao kinachoitwa *Utenzi wa Uhuru wa Kenya* kilichapishwa mwaka 1972 na kumpatia sifa kubwa kwani kilishika nafasi ya kwanza nchini Kenya katika mashindano ya Tunzo ya Fasihi ya Jomo Kenyatta mwaka 1973.

Mwaka 1975 alitunga na kuchapisha kitabu chake cha pili kinachoitwa *Matatu ya Thamani*. Hiki ni kitabu cha hadithi za nasaha. Na mwaka 1988 aliandika kitabu chake kengine kinachoitwa *Ushindi wa Maisha*.

Mzee Salimu Ali Kibao alihamia Dar es Salaam mwaka 1970 kuendelea na kazi yake ya ushoni na mwaka 1976 alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) akikiwakilisha Chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA). Pia amekuwa mjumbe wa Halmashauri ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili na Mjumbe wa Kamati ya Utendaji na Kamati ya Kusanifu Lugha za BAKITA hadi kifo chake. Hayati Kibao alikuwa pia Makamu wa Katibu Mkuu wa UKUTA.

Katika maadhimisho ya miaka 10 ya uhuru wa Tanganyika, 1971, Bw. Kibao alishiriki na kushinda katika fani ya mashairi. Muswada wa kitabu chake cha *Utenzi wa*

Tom Mboya haukuchapishwa. Mswada wake wa *Ngano za Hekima* ulichapishwa na UNESCO miaka ya 1980.

Katika vipindi vya redio ambako alianza kushiriki tangu mwaka 1972, amesikika katika “Lugha ya Taifa”, “Mbinu za Kiswahili” ambacho baadaye kilibadilishwa jina na kuitwa “Ulimwengu wa Kiswahili” na “Ngano za Ushairi.”

Aidha katika uhai wake, miaka 16 iliyopita, alishiriki katika mashindano ya kutafuta shairi bora kwa ajili ya Tamasha la Utamaduni wa Mtu Mweusi lililofanyika mjini Lagos, Nigeria. Hadi leo, hajalipwa na Serikali zawadi yake ya sh. 7,500 (za mwaka 1983) kwa ushindi wa shairi lake. Hayati Salim A. Kibalo alikuwa mtafiti wa fasihi na lugha ya Kiswahili. Mwaka 1993 alishirikiana na watafiti wa TUKI, M.M. Mulokozi na T.S.Y. Sengo, kufanya utafiti kuhusu historia na maendeleo ya ushairi katika Mkoa wa Tanga.

Hayati Kibao alibahatika kupata watoto 13; walio hai ni 9, na wajukuu ni wawili. Ndoa yake ya kwanza ilikuwa mwaka 1957, na aliishi na mke huyo kwa miaka saba bila ya mtoto. Alioa tena mwaka 1964 na kupata watoto tisa baada ya kuishi na mke huyo kwa miaka 15 na kutengana. Mke aliyemwoa 1978 amepata naye watoto wanne na ndiye aliyemwacha kizuka.

Amekuwa akitumia muda wake mwingi kutetea hadhi ya Kiswahili na kutaka kitumike kuwa lugha ya kufundishia elimu ya juu, yaani sekondari na vyuo vya elimu.

“Lugha ya Kiswahili ina maneno mengi yanayojitosheleza... mbona Japan, China, Ufaransa, Urusi na kwingineko watu wamepiga hatua kubwa katika maendeleo ya sayansi na teknolojia bila ya kutumia lugha ya Kiingereza? Mbona wanatengeneza vitu kwa lugha zao? Mtu akiwa na elimu ya kutengeneza dirisha kwa Kiingereza, hata anayejua Kiswahili naye anaweza kutengeneza dirisha hilo....”

Aliwahi kutamka “Elimu ni tofauti na lugha. Hawa wasomi ingawa hawajui matumizi na maana ya maneno ya Kiswahili, hawataki kabisa kutuuliza sisi tunaofahamu lugha hii. Nadhani wanafanya hivyo kwa kutudharau, kwani wanatuona sisi hatuna elimu kama yao.” Haya aliyasema wakati wa uhai wake akilalamikia matumizi ya maneno *wajibu*, *dhima* na *dhambi*.

Alifariki Jumamosi tarehe 16.1.99 na kuzikwa Jumapili 17.1.99 katika makaburi ya Kisutu, Dar es Salaam.

Mohamed Mwinyi
(BAKITA)